Mradi wa Tasaf wawezesha tani 1.8 za samaki kuvunwa

Na Alexander Sanga, Mwanza

TANI 1.8 za samaki zimevunwa kupitia mradi wa ufugaji wa samaki kwa mfumo wa vizimba unaotekelezwa na kaya masikini mkoani Mwanza.

Mpango huo ni wa Kunusuru Kaya Maskini ulio chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kutoka vikundi vya Temeke na Maliganganya vilivyopo Kata ya Bugogwa, Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela.

Samaki hao walifugwa kwa kipindi cha miezi minane na kuvunwa kwa awamu mbili, ambapo thamani ya mavuno hayo inakadiriwa kufikia zaidi ya Sh milioni 15.

Akizungumza juzi wakati wa uvunaji, Mratibu wa Tasaf Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela, David Lugenzi alisema mafanikio ya mradi huo yametokana na usimamizi mzuri wa vikundi, nidhamu ya wanakikundi pamoja na elimu waliyopewa kuhusu ufugaji wa samaki wa vizimba.

Alieleza kuwa Tasaf inaendelea kusimamia miradi ya walengwa kuhakikisha inaleta tija na matokeo chanya kwa jamii.

Alisema mradi huo ni miongoni mwa miradi ya kiuchumi inayolenga kuwawezesha walengwa wa Tasaf kujiondoa kwenye umasikini kwa kuongeza kipato na kuimarisha maisha yao.

Lugenzi alitoa pongezi kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada anazozifanya kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia programu za Tasaf, akisema serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika miradi ya uzalishaji mali.

Msimamizi wa vikundi vya Tasaf wa Mtaa wa Kayenze Ndogo, Rutigalida Bihengo alisema samaki hao walifugwa kwa kipindi cha miezi minane na mradi umeleta mafanikio makubwa kwa wanakikundi.

Alieleza wanufaika wamejifunza mbinu bora za ufugaji, usimamizi wa chakula cha samaki pamoja na utunzaji wa vizimba.

"Tunaishukuru serikali pamoja na viongozi wa wilaya kwa kuleta mradi huu katika eneo letu. Mradi umeongeza kipato kwa wanakikundi na umetupa ujasiri wa kuendelea kuwekeza zaidi kwenye ufugaji wa samaki," alisema.

Naye Modesta Chigugu mnufaika wa mpango huo wa kupunguza umasikini kutoka kikundi cha Temeke, alisema tangu kuanza kwa mradi huo wamefanikiwa kuvuna samaki mara mbili, hali inayoonesha ufugaji wa vizimba una tija kubwa endapo utasimamiwa ipasavyo.